(4) Waziri atateua watu wenye ujuzi na uzoefu katika masuala yanayohusiana na udhibiti wa dawa za kulevya au watu ambao mchango wao unaweza kuwa na msaada mkubwa katika utayarishaji na utekelezaji wa sera ya Taifa kuhusu dawa za kulevya, kuwa wajumbe wa Kamati ya Ushauri.

(5) Mwenyekiti anaweza kumualika mtu yeyote kuhudhuria mojawapo ya kikao cha Kamati kwa lengo la kuisaidia kufikia maamuzi, hata hivyo, mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

(6) Muda wa kukaa madarakani kwa kila mjumbe wa Kamati utakuwa ni miaka mitatu na anaweza kuteuliwa kwa kipindi kingine.

Wajibu wa kudhibiti dawa za kulevya

10.-(1) Serikali itachukua hatua stahiki kwa lengo la kuzuia na kupambana na matumizi ya dawa za kulevya za nakotiki na saikotropiki pamoja na usafirishaji haramu.

(2) Hatua zinazoweza kuchukuliwa na Serikali kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), zitajumuisha-

- (a) kuratibu shughuli zinazofanywa na maafisa na taasisi chini ya Sheria hii na Sheria yoyote kuhusiana na utekelezaji wa masharti ya Sheria hii na matakwa ya mikataba ya kimataifa;
- (b) Kusaidia mamlaka husika katika nchi za nje na mashirika ya kimataifa kwa lengo la kuwezesha shughuli za uratibu ili kuwa na mikakati ya pamoja ya kudhibiti matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevya za nakotiki na saikotropiki;
- (c) Kutambua, kutibu, kuelimisha, kuwaweka katika uangalizi maalumu baada ya tiba na kuwarudisha katika hali ya kawaida na kuwafanya warudi na wakubalike katika jamii; na
- (d) masuala mengine kama ambavyo Serikali itaona inafaa katika kuleta ufanisi katika kuzuia na kupambana na matumizi ya dawa

dawa za kulevya za nakotiki na saikotropiki.

SEHEMU YA TATU

KATAZO LA UMILIKI NA USAFIRISHAJI WA DAWA ZA
KULEVYA ZA NAKOTIKI NA SAIKOTROPIKI PAMOJA NA
KILIMO CHA MIMBA INAYOZALISHA DAWA ZA KULEVYA

Katazo la
kilimo cha
mimea
inayozalisha
dawa za
kulevya

11.-(1) Mtu yoyote ambaye:

- (a) analima mimea iliyokatazwa;
- (b) anamiliki au kusambaza mbegu zinazozalisha dawa za kulevya;
- (c) anamiliki, ana mamlaka au msimamizi wa jengo, eneo au mahali, anaruhusu maeneo haya kutumika kwa ajili ya kilimo cha mimea inayokatazwa;
- (d) anazalisha, kumiliki, kuuza, kununua, kusafirisha, anaingiza ndani ya Tanzania Bara, anasafirisha kwenda nje ya Tanzania Bara, anatumia au anafanya jambo lolote au anazembea kufanya jambo lolote linalohusiana na mimea iliyokatazwa au mimea ya kuzalisha dawa za kulevya akaenda kinyume na masharti ya Sheria hii,

atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atapewa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka thelathini.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki neno “kilimo” linajumuisha “ukusanyaji”.

Mamlaka
kutoa idhini,
kudhibiti na
kusimamia
kilimo,

12.-(1) Mamlaka inaweza kwa kupitia kanuni-

- (a) kutoa vibali na kusimamia-
 - (i) kilimo au ukusanyaji wa sehemu yoyote ya mmea wa koka, mmea wa

uzalishaji au
uuzaji wa
kasumba au
majani ya
koka

- bangi, mmea wa mrungi, usafirishaji, uingizaji, Tanzania Bara, utumiaji au ukusanyaji wa majani ya koka kwa niaba tu ya Serikali;
- (ii) kilimo cha mibaruti afyuni kwa matumizi pekee ya Serikali;
 - (iii) uzalishaji na utengenezaji wa kasumba na uzalishaji wa mimea afyuni;
 - (iv) uuzaji wa kasumba na mazalia yake kutoka viwanda vya Serikali kwa ajili ya kusafirisha nje ya au Tanzania Bara kwa wataalam wa kutengeneza dawa; utengenezaji, umiliki, usafirishaji, uuzaji, ununuzi, na utumiaji wa saikotropiki; au
 - (v) utengenezaji wa dawa za viwandani isipokuwa kasumba bila kuhusisha utengenezaji wa dawa ya tiba yenye asili ya kulevya inayotokana na kasumba zilizotengenezwa viwandani ambazo zimetokana na malighafi zinazomilikiwa kihalali na mtengenezaji;
 - (vi) utengenezaji, umiliki, usafirishaji, uuzaji, ununuzi, na utumiaji wa saikotropiki; au
 - (vii) uingizaji Tanzania bara na upitishaji wa dawa za nakotiki na saikotropiki;
- (b) kuagiza jambo lolote muhimu litakaloiwezesha Serikali kudhibiti kikamilifu mambo yaliyoelezwa katika aya (a).
- (2) Kanuni zilizotayarishwa na Mamlaka zinaweza kuainisha masharti yanayohusu utoaji leseni, vibali au uzalishaji, utengenezaji, umiliki, usafirishaji,

uingizaji Tanzania Bara na usafirishaji nje ya nchi, uuzaji, ununuzi, matumizi, uhifadhi, usambazaji, kuharibu au namna ya kupata dawa za nakotiki au saikotropiki.

Kutoshikiliwa kwa dawa za nakotiki na saikotropiki

13. Bila kujali jambo lolote linalokwenda kinyume na yaliainishwa kwenye sheria yeyote au mkataba wowote, ni marufuku kwa dawa za kulevya za nakotiki, saikotropiki au mimea inayokatazwa, kushikiliwa na mtu yeyote kwa ajili ya kukomboa fedha kwa amri ya mahakama yoyote au mamlaka yoyote au vinginevyo.

Masharti ya kutojihusisha na dawa za nakotiki na saikotropiki

14. Mtu yeyote katika Tanzania Bara hatoruhusiwa kujihusisha au kusimamia biashara yoyote ya dawa za nakotiki au saikotropiki zinazopatikana nje ya nchi au kupelekwa kwa mtu yeyote nje ya Tanzania Bara bila idhini au kibali cha Mamlaka na kwa kuzingatia masharti yatakavyotolewa na Mamlaka.

Katazo la kumiliki, kusafirisha, kununua, kutengeneza dawa za nakotiki, saikotropiki na kemikali bashirifu

15.-(1) Mtu yeyote ambaye-

- (a) akikutwa anamiliki au kufanya jambo lolote au kuacha kufanya jambo lolote kuhusiana na dawa za nakotiki au saikotropiki au utayarishaji wenye dawa za kutengenezwa viwandani;
- (b) anasafirisha dawa yoyote ya nakotiki au saikotropiki; na
- (c) kinyume cha Sheria anamiliki, anasafirisha, anachepusha au anajihusisha kwa njia yoyote ile na kemikali bashirifu.

(2) Mtu yeyote anayezalisha, kumiliki, kusafirisha, kupeleka nje ya nchi, kuingiza katika Jamhuri ya Muungano, kuuza, kununua au kufanya kitendo chochote au kuacha kufanya kitendo chochote kuhusiana na dawa za kulevya ambazo hazijaorodheshwa kwenye Jedwali lililopo katika Sheria hii, lakini imethibitishwa kuwa dawa hizo zinaathiri

kama dawa za kulevya, anatenda kosa na akitiwa hatiani atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Umiliki wa mashine, mitambo na maabara za kutengeneza dawa za nakotiki na saikotropiki

16. Mtu yeyote anayemiliki mashine, mtambo, maabara au chombo chochote kwa lengo la kutayarisha, kuzalisha au kutengeneza dawa za nakotiki au saikotropiki, anatenda kosa na akipatikana na hatia atapewa adhabu ya kifungo cha maisha na nyongeza ya faini isiyopungua shilingi milioni mia mbili.

Katazo kumiliki, Kutumia kiasi Kidogo cha Nakotiki na Saikotropiki

17.-(1) Mtu yeyote anayekiuka sharti lolote kwenye Sheria hii au kibali kinachotolewa chini ya Sheria hii, anamiliki kiasi kidogo cha dawa za kulevya aina ya nakotiki au saikotropiki ambacho kimethibitishwa kuwa ni kwa ajili ya matumizi binafsi au anatumia dawa za kulevya aina ya nakotiki na saikotropiki, akitiwa hatiani bila kuathiri chochote kilichopo kwenye Sehemu hii, atawajibika, iwapo-

- (a) dawa za kulevya aina ya nakotiki au saikotropiki anazohusishwa nazo ni kokeini, mafini, diacetyl – mafini au dawa kokeini, mafini, diacetyl – mafini au dawa yoyotya kulevya aina ya nakotiki au saikotropiki itakavyokuwa imeainishwa na Waziri kwenye Gazeti la Serikali, kulipa faini isiyopungua milioni moja au kutumikia kifungo cha miaka mitano au vyote kwa pamoja.
- (b) kama dawa za kulevya husika ni tofauti na zile zinazotajwa katika aya (a), atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi laki tano au kutumikia kifungo cha miaka mitatu au vyote kwa pamoja.

(2) Jukumu la kuthibitisha kuwa kiasi kidogo cha dawa za kulevya alichokutwa nacho mtuhumiwa ni kwa ajili ya matumizi yake binafsi na si kwa ajili ya kuuza au kusambaza kwa watu, litakuwa juu yake.

(3) Neno “kiasi kidogo cha dawa za kulevya” kama lilivyotumika katika kifungu hiki lina maana kiasi kitakachoainishwa na Waziri kwenye miongozo na kanuni.

Katazo la kuvuta, kunusa au kutumia dawa za nakotiki au saikotropiki

18. Mtu ambaye-

- (a) anavuta, ananusa, anajidunga au vinginevyo anatumia dawa yoyote ya kulevya;
- (b) kinyume na sheria na bila kuwa na sababu za msingi, anakutwa katika nyumba, chumba au mahali panapotumika kinyume na Sheria kuvutia, kunusia aina yoyote ya dawa za kulevya; au
- (c) kinyume cha sheria na bila sababu za msingi, anamiliki aina yoyote ya kiko au kifaa au chombo kinachotumika kwa ajili ya kuvuta, kunusa au kwa namna nyingine anatumia dawa za kulevya,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni moja au kifungo cha miaka mitatu au vyote kwa pamoja.

Katazo kwa mmiliki au mtumiaji wa jengo

19.-(1) Mtu ambaye ni mmiliki, anayeishi, au mtu anayehusika na usimamiaji wa jengo, nyumba, boma, kiwanja, chombo cha usafirishaji, hatoruhusu vitumike kwa lengo la kutayarisha dawa za kulevya au kwa ajili ya kuvuta, kuuza, kujidunga, kunusa au kutumia dawa hizo kwa namna yoyote ile isipokuwa tu kwa kibali kutoka mamlaka husika.

(2) Mtu yeyote atakaye kwenda kinyume na kifungu kidogo cha (1), anatenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni tano au kifungu kisichopungua miaka mitatu au vyote kwa pamoja.

Katazo la
kumsababishia
mtu atumie
Dawa za
nakotiki
saikotropiki

20.-(1) Mtu yeyote ambaye-

- (a) anatoa dawa za nakotiki au saikotropiki au anasababisha au kuruhusu dawa hizo zitolewe isipokuwa afisa muidhiniwa au ni daktari wa binadamu au daktari wa meno ambaye anatoa dawa hizo kwa mujibu wa maadili ya taaluma yake na viwango vilivyoruhusiwa;
- (b) anaye mwekea mtu dawa za kulevya kwenye chakula au kinywaji au anatomia njia yoyote ile kumwekea dawa hizo bila ya mtumiaji kujua; au
- (c) anauza, anasambaza au kupata dawa za nakotiki na saikotropiki kwa cheti cha daktari huku akijua au akiwa na sababu za kuamini kuwa cheti hicho kimegushiwa au kimepatikana isivyo halali au kimetolewa zaidi ya miezi sita tangu cheti kiandikwe,

anatenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni ishirini au kifungu kisichopungua miaka thelathini au vyote kwa pamoja.

(2) Endapo kosa limetendeka chini ya kifungu kidogo cha (1):

- (a) mashuleni au kwenye taasisi za elimu, vituo vya huduma za kijamii au maeneo yanayozunguka taasisi hizo; au
- (b) waathirika ni watu walio chini ya miaka kumi na nane mtu huyo anatenda kosa na

akipatikana na hatia atatumikia kifungo kisichopungua miaka thelathini.

Wakulima
kwenda
kinyume na
masharti ya
vibali na leseni

21. Mtu yeyote aliyepewa leseni na Serikali kulima mimea ya mibaruti afyuni na isivyo halali akauza au akashindwa kuitunza inavyotakiwa mimea au sehemu ya mimea hiyo, anatenda kosa na akipatikana na hatia atatakiwa kulipa faini ya shilingi milioni kumi na tano au kifungo kisichopungua miaka thelathini au vyote kwa pamoja, na mahakama inaweza, kwa sababu zitakazoelezwa katika hukumu kutoa adhabu isiyopungua faini ya shilingi milioni thelathini iwapo mkosaji amerudia kosa.

Kukiuka
masharti ya
leseni au kibali

22. Endapo mwenye leseni, kibali au idhini iliyotolewa kulingana na matakwa ya Sheria hii-

- (a) anaacha bila sababu za msingi kutunza mahesabu au kuwasilisha marejesho kwa mujibu wa Sheria hii;
- (b) bila sababu za msingi anashindwa kutoa, kutunza akaunti za mahesabu au kuwasilisha marejesho kwa mujibu wa Sheria hii;
- (c) kutunza kumbukumbu za mahesabu au kutoa taarifa ambazo anajua au anazo sababu kuamini kuwa taarifa alizotoa si sahihi;
- (d) kufanya tendo lolote kwa makusudi huku akifahamu kuwa anavunja masharti ya leseni, kibali au ruhusa ambavyo adhabu zinatolewa katika Sheria hii,

anatenda kosa na akipatikana na hatia atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi milioni ishirini na tano au

kutumikia kifungo kisichopungua miaka thelathini au vyote kwa pamoja na nyongeza ya kufutiwa leseni au kibali chake.

Kufadhili
vitendo
haramu

23. Mtu ambaye anajua moja kwa moja au anajua kwa namna nyingine kuwa anafadhili vitendo vilivyoainishwa katika kifungu cha 15 au kumhifadhi mtu yeyote anayejihusisha na vitendo husika, anatenda kosa na akipatikana na hatia atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi bilioni moja na nyongeza ya kifungo cha maisha.

Katazo la
kusaidia
kutendeka
kwa
makosa

24. Bila kujali yaliyomo katika sheria nyingine; mtu yeyote atakaye-

- (a) kula njama na mtu yeyote kutenda kosa;
- (b) shawishi, chochea, saidia, ficha au kujaribu kushawishi, kusaidia, shirikiana, au kimficha mtu alietenda kosa;
- (c) sababisha au kujaribu kusababisha kufanyika kwa kosa chini ya sheria hii;
- (d) vinginevyo moja kwa moja au vinginevyo anajua anahusika na utendaji wa kosa chini ya Sheria atashitaiwa kwa makosa husika kama mkosaji mkuu,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atatakiwa kulipa faini ya shilingi milioni tano au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka thelathini au vyote kwa pamoja.

Maandalizi au
jaribio la
kutenda kosa

25. Endapo mtu atajaribu kutenda au kuacha kufanya kitu kinachopelekea utendaji wa kosa chini ya Sehemu hii na kutokana na mazingira yaliyopo anaweza akachukuliwa kuwa alikusudia kutimiza nia ya kutenda kosa hilo lakini alizuiwa na mazingira tofauti na nia yake, atawajibika kutumikia kifungo si chini ya nusu ya kifungo

anachostahili mtu ambaye angeweza kuadhibiwa kama angetenda kosa hilo, na kulipa nusu ya faini yote ambayo angelitenda kama angelitenda kosa hilo.

Kurudia
kutenda kosa

26.-(1) Mtu yeyote aliyetiwa hatiani kwa makosa chini ya Sheria hii, akitiwa hatiani kwa kosa jingine na kwa kila kosa linalojirudia atatakiwa kulipa faini ya shilingi milioni kumi au kifungo cha maisha.

(2) Endapo mtu atahukumiwa chini ya vifungu vya 19, 20 na 25, na Mahakama yenye mamlaka nje ya Tanzania Bara chini ya sheria yoyote inayofanana na masharti ya sheria yetu kuhusiana na kutiwa hatiani, atashughulikiwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) kama vile amehukumiwa na Mahakama ya Tanzania Bara.

Adhabu
kwa makosa
ambayo
adhabu zake
haziainishwa
kwenye Sheria
hii

27. Mtu yeyote ambaye anakiuka masharti yaliyomo kwenye Sheria hii au masharti ya leseni, kibali au idhini iliyotolewa chini ya Sheria hii, ambapo hakuna adhabu mahsusi iliyoaainishwa katika Sehemu hii, akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi milioni ishirini au kifungo kisichozidi miaka thelathini au vyote kwa pamoja.

Wajibu wa
kuthibitisha
kosa

28.-(1) Katika uendeshaji wa mashauri ya kumiliki, kujihusisha na kusafirisha, kuuza, kilimo, ununuzi, utumiaji au kufadhili dawa za nakotiki au saikotropiki, jukumu la kuthibitisha kuwa dawa za nakotiki au saikotropiki zilimilikiwa, kuhusishwa, kusafirishwa, kuuzwa, kulimwa, kununuliwa, kutumiwa au kufadhiliwa kwa mujibu wa masharti ya leseni, kibali au mamlaka yaliyotolewa chini ya Sheria hii, Miongozo, Kanuni au amri, litakuwa jukumu la mshitakiwa.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), itakuwa ni utetezi kwa mtu yeyote aliyeshitakiwa kwa kosa la kujihusisha na umiliki wa dawa za nakotiki au saikotropiki iwapo ataithibitishia na kuiridhisha Mahakama kuwa umilikaji wa dawa hizo za nakotiki au saikotropiki ulizingatia mazingira ya tukio kwa umakini.

Makosa yasiyo
na dhamana

29.- (1) Afisa polisi mkuu wa kituo au afisa wa Mamlaka au mahakama ambapo mtuhumiwa amepelekwa au kushitakiwa haitatoa dhamana kwa mtuhumiwa huyo endapo-

- (a) Mtuhumiwa anashitakiwa kwa kosa la kujihusisha na usafirishaji wa dawa za kulevya aina ya amfetamini, heroini; kokeini, mandrax, mofini, bangi iliyosindikwa, kasumba na dawa nyingine yoyote ya kulevya yenye uzito wa kuanzia gram mia mbili au zaidi;
- (b) mtuhumiwa anashitakiwa kwa kosa la kujihusisha na usafirishaji wa bangi, mirungi na aina yoyote ya mmea uliokatazwa wenye uzito wa kilogram mia moja au zaidi; na
- (c) kwa kemikali bashirifu zenye uzito wa lita thelathini au uzito wa kilogram mia moja katika umbo yabisi.

(2) endapo kutakuwa na mkinzano wowote katika masuala yanayohusu uzito, aina ya kemikali au masuala yoyote yanayofanana na hayo katika kifungu hiki, uzito, aina ya kemikali au kitu chochote kinachohusiana na vitu hiyo, majibu ya Mkemia wa Serikali ndiyo yatakayotambuliwa rasmi.

(3) Masharti ya kutoa dhamana kama yaliyoainishwa chini ya kifungu cha 148 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, yatatumika sambamba kwa Omakosa yote chini ya Sheria hii.

Makosa ya kampuni

30.-(1) Endapo kosa limetendwa chini ya Sheria hii na Kampuni, kila mtu ambaye wakati kosa linatendeka, alikuwa anaongoza au anasimamia shughuli za uendeshaji wa kampuni atachukuliwa kuwa ametenda kosa na atastahili kushitakiwa na kuadhibiwa ipasavyo.

(2) Kifungu cha (1) hakitasababisha mtu yeyote kupewa adhabu yoyote iwapo atathibitisha kwamba kosa lilitendeka bila yeye kufahamu au alifanya jitihada kuzuia kutendeka kwa kosa hilo.

(3) Bila kujali kifungu kidogo cha (2), pale ambapo kosa chini ya sehemu hii limefanywa na kampuni na kuthibitishwa kwamba kosa limetendeka kwa ruhusa au nia ovu, au imesababishwa na uzembe wa mkurugenzi yeyote, meneja, katibu au afisa mwingine wa kampuni, mkurugenzi huyo, meneja, katibu au afisa mwingine wa kampuni atashtakiwa na kuadhibiwa ipasavyo na kampuni hiyo itafutiwa kibali au kutaifishwa.

Kuachiwa kwa baadhi ya watumiaji wa dawa za kulevy kwa lengo la kupata tiba

31.-(1) Endapo muathirika atakapotywa hatiani kwa kosa chini ya kifungu cha 18 na mahakama ambayo imemtia hatiani imeona kwamba kutokana na-

- (a) umri, tabia au historia ya mtumiaji;
- (b) hali ya mwili na akili ya mkosaji, kwa kadiri itakavyoona inafaa;

hivyo bila ya kuathiri chochote kilichopo katika Sheria hii au sheria nyingine yoyote mahakama yaweza badala ya kutoa adhabu ya kifungo, kwa ridhaa yake ikaelekeza kwamba mtumiaji huyo aachiwe kwa ajili ya kupata tiba ya kuondoa sumu mwilini katika hosipitali au taasisi inayoendeshwa na kutambuliwa na Serikali

(2) Endapo muathirika ataachiwa kwa ajili ya kupata matibabu, atapaswa kuingia makubaliano kama itakavyoelekezwa na Mamlaka, akiwa na wadhamini au la, kumuelekeza kuja na kutoa taarifa inayohusu matibabu yake kwenye mahakama kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu na katika kipindi hicho hatokuwa kutenda kosa lolote chini ya Sehemu hii.

(3) Endapo mhalifu atashindwa kufuata masharti ya kuacha kutenda kosa baada ya kuachiwa na mahakama kwa ajili ya kwenda kupata matibabu kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2), mahakama inaweza kumuamuru mtuhumiwa huyo kwenda mahakamani kwa ajili ya kuhukumiwa.

SEHEMU YA NNE TARATIBU ZA UKAMATAJI

Kutumika kwa
Sheria ya
Mwenendo wa
Makosa ya
Jinai na
kuweka
marekebisho
muhimu

32.-(1) Maafisa wa Mamlaka watakuwa na uwezo wa kukamata kupekuwa, kushikilia na kufanya upelelezi kuhusiana na makosa yaliyoainishwa chini ya Sheria hii.

(2) Masharti ya sheria nyingine yeyote inayotumika katik Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusiana na mamlaka na wajibu wa kuchunguza, kukamata, kupekua na kushikilia vitu kwa maafisa wa jeshi la polisi, afisa forodha, au mtu mwingine mwenye mamlaka

ya kukamata, yatatumika pia katika sheria hii.

(3) Afisa wa Mamlaka atakuwa na uwezo wa kumkamata, kupekua, kuchunguza, kushikili na kuchukua maelezo yanayohusiana na jambo lolote chini ya Sheria hii, kama vile ni afisa wa polisi anayetokeleza majukumu na kutimiza wajibu wake chini ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Ushuru wa Forodha au Sheria nyingine yoyote inayotoa uwezo wa kukamata na kushikilia vitu.

(4) Matakwa ya Sheria nyingine yoyote inayotumika katika jamhuri ya Muungano kuhusiana na mamlaka na wajibu wa kuchunguza, kukamata, kupekua, kushikilia na kuchukua maelezo kwa afisa wa polisi, maafisa forodha, au mtu mwingine mwenye mamlaka ya kukamata, yatatumika na afisa anayetumia Sheria hii.

(5) Kitu chochote kilichokamatwa au kuchukuliwa maelezo na afisa kitapokelewa mahakamani kama ushahidi.

(6) Afisa yeyote aliyetajwa katika kifungu kidogo cha (1), muda wowote anaweza-

- (a) kuingia na kupekua jingo lolote, chombo chochote cha uchukuzi au mahali;
- (b) iwapo kuna upinzani, kuvunja mlango wowote au kuondoa kizuizi chochote cha kuingia mahali hapo.
- (c) Kukamata dawa yoyote na vifaa vyote vilivyotumika katika kutengeneza dawa au kifaa chochote, au chombo cha usafirishaji akiamini kuwa vyombo au vifaa hivyo vimetumika katika utendaji wa makosa chini ya Sheria hii.
- (7) Endapo afisa anachukua taarifa au kurekodi sababu za kukamata bila kuchelewa kupeleka nakala ya taarifa au rekodi hiyo kwa mkuu wake wa kazi.

Utaribu wa
kukamata ambapo
utaifishaji
hauwezekani

33. Pale ambapo haiwezekani kushikilia vitu vikiwemo mazao yaliyopo ambayo yanastahili kutaifishwa, afisa yeyote aliyeidhinishwa chini ya kifungu cha 33 anaweza kumpatia mmiliki au mtu mwenye kumiliki vitu hivyo na kuamuru kwamba hataondoa, au kuachana na vitu hivyo au vinginevyo kujihusisha na vitu hivyo isipokuwa kwa ruhusa ya afisa huyo.

Jukumu kwa
wamiliki wa ardhi
kutoa taarifa za
mazao ya dawa za
kulevya
yaliyolimwa isivyo
halali

34. Kila mmiliki, anayeishi, au mtu anayesimamia ardhi yoyote, nyumba au sehemu atatoa taarifa haraka kwa afisa yeyote wa polisi au afisa wa idara zilizotajwa katika kifungu cha 33 juu ya uwepo wa mazao yanayozalisha dawa za kulevya, dawa za nakotiki au saikotropiki ambazo zimelimwa isivyo halali, imezalishwa au kutengenezwa ndani ya ardhi yake, jengo au eneo na kila mmiliki ambaye anajua lakini anapuuza kutoa taarifa hiyo, anatenda kosa na akipatikana na hatia atatakiwa kulipa faini ya shilingi milioni ishirini, au kifungo cha miaka thelathini au vyote kwa pamoja.

Mamlaka ya
kushikilia mazao
yaliyolimwa
isivyo halali

35. Afisa yeyote mwenye mamlaka chini ya Sheria hii, anaweza kuamuru kushikiliwa kwa mazao ya mimea ya mibaruti afyuni, mimea ya bangi, mirungi, mimea jamii ya koka au mimea mingine ya dawa za kulevya iwapo anaamini kuwa imelimwa isivyo halali, na anaweza kutoa amri hiyo, ikiwemo amri ya kuharibu mimea hiyo kama atakavyoona inafaa.

Mamlaka kuamuru
baadhi ya dawa
kuharibiwa

36.-(1) Mamlaka inaweza, kwa kuzingatia hali ya hatari ya dawa za nakotiki au saikotropiki au urahisi wa kuweza kuibiwa, kubadilishwa, ufinyu wa mahali maalum pa kuhifadhia, sehemu au mambo mengine yanayoweza kuzingatiwa, kwa Notisi katika *Gazeti* la Serikali, kuamuru dawa hizo za nakotiki na saikotropiki ziharibiwe kwa utaratibu kama Mamlaka itakavyoamua baada ya kufuata taratibu zilizoainishwa.

(2) Endapo dawa za kulevya aina ya nakotiki na saikotropiki zimekamatwa, afisa aliyekamata dawa hizo au dawa za saikotropiki ataandaa orodha ya kuonyesha taarifa zinazohusu-

- (a) aina ya dawa za nakotiki au saikotropiki, ikiwa na maelezo kuhusiana na aina, kiasi, jinsi ilivyopakiwa, alama, namba;
- (b) alama yoyote ya kuitambua dawa ya nakotiki au saikotropiki;
- (c) jinsi ilivyofungwa,
- (d) nchi ilipotoka; na
- (e) vitu vingine ambavyo afisa ataona inafaa kwa ajili ya utambuzi wa dawa za nakotiki au saikotropiki katika mashauri yoyote chini ya Sheria hii.

(3) Afisa aliyekamata dawa hizo au dawa za saikotropiki atatuma maombi kwa Hakimu yeyote mwenye mamlaka chini ya Sheria hii kwa madhumuni ya-

- (a) kujiridhisha na usahihi wa orodha iliyotayarishwa;
- (b) kupiga picha dawa za kulevya mbele ya Hakimu na kuthibitisha kuwa picha hizo ni za kweli;

(c) kuruhusu kuchukua sampuli ya dawa hizo au vitu mbele ya Hakimu huyo, na kuthibitisha usahihi wa orodha ya sampuli iliyochukuliwa.

(4) Pale ambapo ombi limefanywa chini ya kifungu kidogo cha (3), Hakimu atakubali mara moja ombi hilo.

(5) Bila ya kuathiri masharti yaliyomo katika Sheria ya Ushahidi au Sheria ya Mwenenedo wa Makosa ya Jinai, kila Mahakama inayohukumu kosa chini ya Sheria hii, itachukua orodha, picha za dawa za nakotiki au saikotropiki na orodha ya sampuli zilizochukuliwa chini ya kifungu kidogo cha (3) na kuthibitishwa na Hakimu, kama ushahidi wa awali kuhusiana na kosa hilo.

Sura ya 6 na
20

Umuhimu wa
maelezo katika
mazingira fulani

37.-(1) Maelezo yaliyotolewa na kusainiwa mbele ya afisa mwenye mamlaka chini ya kifungu cha 51 cha Sheria hii, kuchunguza makosa, katika na wakati wa mahojiano au mwenendo wa kesi na afisa huyo, yatakuwa ni muhimu kwa madhumuni ya kuthibitisha, shitaka lolote la kosa lolote chini ya Sheria hii na ukweli wa maelezo yaliyomo-

(a) endapo mtu aliyetoa maelezo amefariki dunia au hawezi kupatikana au hawezi kutoa ushahidi au amezuiwa na adui yake au uwepo wake hayawezekani pasipokuwa na ucheleweshaji au gharama ambapo kutokana na mazingira ya kesi mahakama inaona hakuna haja; au

(b) endapo mtu aliyetoa maelezo anahojiwa kama shahidi katika kesi iliyopo mahakamani; na mahakama ina maoni ya kwamba kwa kuangalia mazingira ya kesi maelezo hayo yatachukuliwa kama ushahidi ili kuhakikisha haki inatendeka.

(2) Endapo kutatokea kukinzana kati ya masharti ya kifungu hiki na vile vya Sheria ya Ushahidi, masharti ya kifungu hiki yatakuwa na nguvu.

Kuchukuliwa kuwa unamiliki vitu haramu

38. Katika mashitaka chini ya sheria hii, inaweza kuchukuliwa, isipokuwa kama itathibitishwa kwamba mtuhumiwa ametenda kosa chini ya Sehemu hii ya Tatu

- (a) madawa ya nakotiki au saikotropiki;
- (b) baruti afuyuni, mimea ya bangi, mirungi au mimea ya koka inayolimwa katika ardhi yoyote;
- (c) kifaa chochote kilichobuniwa maalum au aina yoyote ya chombo kilichochukuliwa maalum kwa ajili ya kutengenezea aina yoyote ya dawa za nakotiki au saikotropiki; au
- (d) malighafi yoyote iliyotumika kutengenezea dawa za nakotiki au saikotropiki, au mabaki yoyote ya vitu vilivyobaki kwenye dawa zilizotengenezwa nakotiki au saikotropiki kushindwa kuthibitisha umiliki wake.

Afisa muidhiniwa kusimamia vitu vilivyokamatwa

39.-(1) Afisa aliyeidhinishwa chini ya kifungu cha 44 atachukua hatua ya kuweka katika uangalizi, kusubiri amri ya Hakim, mkazi na kuruhusu afisa aliyekamata vitu hivyo ambaye amekaimishwa kufanya hivyo, kuvipiga muhuri vitu hivyo au kuchukua sampuli

za vitu hivyo na sampuli hizo zilizochukuliwa zitafungwa na lakiri ya ofisi ya ofisa huyo.

(2) Afisa yeyote atakayeshindwa kufuata masharti yanayohusu uhifadhi wa vitu vilivyokamatwa na akasababisha kupotea kwa vitu hivyo anatenda kosa na akipatikana na hatia, atatakiwa kulipa faini ya shilingi milioni kumi na tano au kifungo cha miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Wajibu wa maofisa kusaidiana

40. Maafisa wote waliyotajwa katika Sheria hii, ambao kazi au mamlaka mahsusi au ya jumla wamepewa chini ya Sheria hii baada ya kupewa taarifa au kutakiwa kufanya hivyo, watapaswa kisheria kusaidiana katika kutekeleza masharti ya sheria hii.

Ukamataji na utafishaji kutolewa taarifa ndani ya masaa arobaini na nane

41. Endapo mtu yeyote amekamata watuhumiwa au vitu chini ya Sheria hii anatakiwa ndani ya masaa arobaini na nane baada ya kukamata au kushikilia vitu hivyo kutoa taarifa kamili ya maelezo ya kukamatwa huko au kushikilia huko kwa afisa wa juu anayemfuatia.

Udanganyifu katika utwaaji, uingiaji na ukamataji

42.-(1) Afisa yeyote ambaye katika kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya Sheria hii-

- (a) bila ya kuwa sababu zozote za kutilia shaka, anangia au kupekua au kusababisha kuingia au kukagua jengo lolote, chombo cha uchukuzi au mahali;
- (b) bila ya ulazima wowote anakamata mali ya mtuyeyote kwa lengo la kukamata kitu au kufanya ukaguzi wa madawa ya nakotiki au saikotropiki au vitu vingine

vinavyopaswa kutaifishwa chini ya sheria hii, au kushikilia nyaraka yoyote au kitu kinachoweza kushikiliwa chini ya sheria hii; au

- (c) bila ya sababu anamzuia, anamkagua au kumkamata mtu yeyote,

atatenda kosa na akipatikana na hatia atatakiwa kulipa faini isiyozidi shilingi milioni mbili au kifungo kwa kipindi cha mwaka mmoja au vyote kwa pamoja.

(2) Mtu ambaye kwa hiari au kwa nia ovu anatoa taarifa za uongo na kusababisha kukamata au kufanyika kwa ukaguzi chini ya Sheria hii, anatenda kosa na akipatikana na hatia atatakiwa kulipa faini isiyozidi shilling milioni moja au kifungo cha miezi sita au vyote kwa pamoja.

Afisa anayeshindwa kutekeleza majukumu kufanya kazi yake au kumsaidia mhalifu

43.-(1) Afisa ambaye amepewa jukumu lolote chini ya Sheria hii-

- (a) anakataa kufanya kazi ya ofisi yake, isipokuwa kama ana sababu za msingi za kufanya hivyo;
- (b) amepewa uangalizi wa muathirika yeyote au mtu yeyote ambaye anashitakiwa kwa kosa chini ya Sheria hii anamwachia au kusababisha kutoka.
- (c) kwa hiari anasaidia katika au anaachia kwa makusudi katika, kuvunjwa kwa masharti yoyote chini ya Sheria hii, anatenda kosa na akipatikana na hatia atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua miaka miwili au vyote kwa pamoja.

(2) Maelezo “afisa” katika kifungu hiki yanajumuisha mtu aliyeajiriwa hospitalini au taasisi inayoendeshwa au kutambuliwa na Serikali kwa ajili ya kutoa usugu wa matumizi ya dawa za kulevy au sumu.

(3) Mahakama haitatambua kosa chini ya kifungu kidogo cha (1) isipokuwa kwa malalamiko ya maandishi yaliyotolewa na Mamlaka.

Mamlaka ya
kutaifisha kifaa au
kitu kinachohusiana
na kosa

44-(1) Endapo kosa chini ya Sehemu ya Tatu limetendeka, madawa ya nakotiki, saikotropiki, mibaruti afuyuni, mimea ya kokeini, mirungi, mimea ya bangi, malighafi zinazotumika, vifaa na vyombo kuhusiana na kosa lililotendwa, vitataifishwa.

(2) Dawa zozote za nakotiki au saikotropiki ambayo yametengenezwa kihalali, kuingizwa au kupelekwa nje ya Tanzania Bara, kusafirishwa, kutengenezwa, kumilikiwa, kutumiwa, kununuliwa au kuuzwa au kwa kongeza madawa yoyote ya nakotiki au saikotropiki ambayo yanatakiwa kutaifishwa na chombo cha kuwekea vitu, kufungia, kufunika ambamo madawa yoyote ya nakotiki au saikotropiki, michanganyo, vifaa au vyombo vinavyoweza kutaifishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) vimepatikana, na ndani yake, vyombo vya kuwekea vitu au kufungia vitataifishwa.

(3) Kitu chochote kianchotumika kwa ajili ya kufichia madawa yoyote ya nakotiki au saikotropiki ambayo yanatakiwa kutaifishwa chini ya sheria hii yatataifishwa.

(4) Endapo madawa ya nakotiki au saikotropiki yameuzwa na mtu mwenye uelewa au kuna sababu za kuamini kwamba madawa au mchanganyiko, utataifishwa chini ya Sheria hii, mapato ya mauzo chini ya Sheria hii nayo yatataifishwa.

Utaifishaji kama mtu hajatiwa hatiani

45.-(1) Katika shtaka la makosa chini ya Sheria hii, ama mtuhumiwa ametiwa hatiani au ameachiwa, Mahakama itaamua kama vifaa au vitu vilivyokamatwa vinatakiwa kutaifishwa.

(2) Endapo kitu chochote chini ya Sheria hii kinaonekana kuwa kinastahili kutaifishwa, lakini mtu aliyetenda kosa linalohusiana na kitu hicho hajulikani au hawezi kupatikana, mahakama inaweza ikachunguza na kuamua, na inaweza, kwa utaratibu unaotumika kuamrisha mali hiyo itaifishwe.

(3) Amri ya kutaifisha kitu au chombo haitatolewa mpaka-

- (a) kupita mwezi mmoja tangu kukamatwa kwake;
- (b) bila ya kumsikiliza mtu yeyote anayedai haki;
- (c) bila ya ushahidi kama upo uliotolewa kuhusiana na madai.

(4) Endapo kitu au kifaa ambacho si dawa ya nakotiki, saikotropiki, mibaruti afyuni, mimea ya koka, mrungi au mmea wa bangi, ambao ni rahisi kuharibika, au iwapo Mahakama inaona uuzwaji wake utakuwa ni kwa faida ya mmiliki, inaweza kuelekeza kiuzwe.

(5) Mtu yeyote ambaye anadai haki ya mali ambayo Mahakama imetaifisha chini ya Sheria hii, anaweza kukata rufaa mahakama ya juu dhidi ya amri ya kutaifisha.

Nyaraka katika mazingira fulani

46. Endapo nyaraka yoyote-

- (a) imetolewa au kuwasilishwa na mtu yeyote au imechukuliwa kutoka kwenye uangalizi au usimamizi wa mtu yeyote chini ya Sheria hii, au chini ya Sheria nyingine yeyote; au
- (b) imepokelewa kutoka sehemu yoyote nje ya Jamhuri ya Muungano, na imethibitishwa na mamlaka hiyo au mtu na kwa namna iliyowekwa na Mamlaka,

wakati wa uchunguzi wa kosa lolote chini ya sheria hii, kama nyaraka hiyo itatolewa katika mwenendo wowote chini ya sheria hii, katika ushahidi dhidi yake au dhidi ya mtu mwingine yeyote ambaye wanashitakiwa pamoja naye, mahakama-

- (i) itaikubali nyaraka katika ushahidi, bila ya kujali kuwa ina mhuri, kama nyaraka hiyo inakubalika katika ushahidi.
- (ii) endapo itawasilishwa chini ya aya ya (a), nayo itapokelewa, isipokuwa kama itathibitika vinginevyo, ukweli wa yaliyomo katika nyaraka hiyo.

Mamlaka ya afisa muidhiniwa kupata taarifa

47-(1) Afisa yeyote ambaye ameidhinishwa chini ya sheria hii, anaweza, wakati wowote wa uchunguzi kuhusiana na kukiuka masharti yoyote ya Sheria hii-

- (a) kutaka taarifa kutoka kwa mtu yeyote kwa madhumuni ya kujiridhisha kama kuna ukiukwaji wowote wa masharti ya Sheria hii; na
 - (b) kutamka ya kwamba mtu yeyote kutoa au kupeleka nyaraka yoyote au kitu kitakachotumika au muhimu kuhusiana na uchunguzi.
- (2) Afisa anayetokeleza mamlaka aliyopewa chini ya masharti ya Sheria hii, hatalazimishwa kusema wapi alipopata taarifa juu ya kutendeka kwa kosa.

Taratibu za
Ukamataji

48.-(1) Taratibu za ukamataji na uwezo waliyopewa maafisa wa Mamlaka chini ya Sehemu hii yatatumika kama yalivyo.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) afisa wa Mamlaka au vyombo vingine vya utekelezaji ambaye-

- (a) atakamata mtuhumiwa kwa:
 - (i) kumgusa mtu mkono au kumweka chini ya ulinzi wake mtu aliyekamatwa;
 - (ii) kutoa taarifa kwa mtu aliyekamatwa msingi au sababu ya kukamatwa kwake na maelezo ya kosa analotuhumiwa kulitenda;
 - (iii) tahadhari katika maandishi na kwa lugha anayoielewa, au kumfahamisha mtuhumiwa haki ya kujibu au kutojibu chochote isipokuwa kwa maswali yanayohusu jina lake na anwani, haki ya kumwita

- wakili wake, jamaa, au rafiki wakati wa mahojiano;
- (iv) kumhoji mtu aliyekamatwa ni jinsi gani anahusiana na dawa za kulevya au kemikali bashirifu au kitu kingine chochote chenye madhara sawa na dawa za kulevya;
 - (v) kumtaka au kuhakikisha kuwa mtuhumiwa anakubali au kukataa kosa kwa maandishi, na inapolazimu, kuchukua maelezo yake mbele ya mlinzi wa amani ndani ya saa ishirini na nne au kwa muda wowote ilimradi muda huo usipitilize sana;
 - (vi) endapo muda wa kuchukua maelezo utakuwa mrefu, afisa atamfahamisha kwa maandishi mtuhumiwa kuhusu kuendelea kwa muda huo na sababu za kuendelea huko;
 - (vii) kuandika tarehe na muda ambao mahojiano yalianza, kukatishwa, kuendelea na kumalizika;
 - (viii) kumruhusu mtuhumiwa kusahihisha, kubadilisha au kuongeza kilichoandikwa, au kufanya marekebisho yoyote, mabadiliko au nyongeza ya kilichoandikwa;

- (ix) endapo mtuhumiwa anatoa maelezo ya kukubali au kukiri kosa au kukana wakati maelezo yanachukuliwa, afisa anayechukua maelezo hayo atayasoma au kuhakikisha kuwa yanasomwa mbele ya mtuhumiwa ambaye atasaini punde tu chini ya mstari wa mwisho wa maelezo hayo na kuruhuru mtu mwingine aliyepo, kama mtu mwingine atakuwepo, atasaini chini ya mstari wa mwisho wa maelezo hayo na kuruhuru mtu mwingine aliyepo, kama mtu mwingine atakuwepo, atasaini kama shahidi wa mtuhumiwa;
- (x) Afisa anayechukua maelezo atajaza hati ya uthibitisho au kuhakikisha kuwa hati hiyo inajazwa ili kuthibitisha usahihi wa maelezo kulingana na fomu iliyopo kwenye Jedwali la tatu la Sheria hii.
- (xi) anafanya upelelezi wa kosa:

(b) anafanya upelelezi wa kosa:

- (i) yeye mwenyewe kwenda kwenye eneo la tukio kupanya upelelezi na atachukua kila kitu kinachohusika kutumika katika kutenda kosa;

- (ii) kuchukua hatua zote muhimu kwa ajili ya kugundua na kukamata kila kitu ambacho kinaweza kutumika kutumika kama ushahidi;
 - (iii) kumhoji kwa mdomo mtu yeyote ambaye ana maelezo na anajua mazingira ya kosa kuepuka lililotendeka;
 - (ii) kuepuka kumfanyia ukatili, vitendo vya kinyama au udhalilishaji mtu aliyekamatwa;
 - (iii) mtu aliyekamatwa anaweza kuruhusiwa kupata tiba au ushauri endapo atakuwa anaumwa au kuumia kwa kuangalia afya yake au maombi atakayotoa;
 - (iv) iwapo mtu aliyekamatwa ni mtoto, mzazi au mlezi wa mtoto huyo afahamishwe kuhusu kushikiliwa kwa mtoto huyo na kosa alilotenda;
 - (v) bila kuchelewa na kwa mujibu wa vifungu vinavyohusiana na dhamana, kumpeleka mtu aliyekamatwa mahakama ya wilaya iliyopo eneo alilokamatwa.
- (c) kufanya upekuzi wa kifaa kilichotumika au kinachohisiwa kutumika katika utendaji wa kosa kwa:
- (i) kusimamisha, pekua na kushikilia chombo chochote, boti, ndege, gari au chombo chochote cha usafiri kinachoshukiwa kubeba kitu chochote kinachohisiwa kuwa dawa za kulevya;

- (ii) kumsimamisha, kumpekua na kumshikilia mtu yeyote ambaye anashukiwa kubeba, kuhamisha, kuhifadhi, kusafirisha, kulima, kuingiza nchini, kutoa nchini au kumiliki kitu chochote kinachodhaniwa kuwa dawa za kulevya;
- (iii) kutoshikilia mtu, chombo chochote, boti, ndege, gari, jengo kwa kipindi cha zaidi maandishi kufuatana na fomu iliyopo kwenye Jedwali la Tatu la Sheria hii kwa madhumuni ya kusaidia uchunguzi zaidi;
- (iv) kama kuna ulazima wa kumkagua mwanamke, ukaguzi huo utafanywa na mwanamke mwenzake;
- (v) kuchukua au kukamata kutoka kwa mtu aliyekamatwa au mtu yeyote kitu chochote kinachohusiana na kosa ambalo amekamatwa nalo, au chochote chenye madhara kama dawa za kulevya;
- (vi) kutoa taarifa ya upekuzi kwa afisa wa Mamlaka aliye juu yake haraka kadiri inavyowezekana;
- (vii) kurekodi na kutoa stakabadhi au kuorodhesha kifaa au kitu chochote kilichokamatwa katika

fomu ya Uchunguzi iliyopo kwenye Jedwali la Tatu la Sheria hii.

(d) kushikilia kifaa kilichotumika au kinachohisiwa kutumika katika kutenda kosa kwa:

- (i) kuhakikisha uwepo na kuchukua maelezo ya watu watakaotoa ushahidi juu ya kifaa kilichoshikiliwa;
- (ii) kurekodi maelezo ya mtu aliyeshikiliwa kuhusu uhusiano wake na kifaa kinachoshikiliwa;
- (iii) kutathmini na kuamua ukubwa, ujazo, wingi, ubora na thamani au thamani iliyokadiriwa ya kifaa kilichoshikiliwa;
- (iv) kukiweka chini ya uangalizi kifaa kianchoshikiliwa kutokana na kitendo chochote cha upotevu, wizi, kusinyaa, kushuka kwa ubora au thamani.

(3) Afisa wa mamlaka ambaye atashindwa kutekeleza majukumu yake au kuacha kufanya kitendo kutokana na uzembe huo, matokeo yake mtu anayetuhumiwa au kushitakiwa kwa kosa linalohusiana na dawa za nakotiki au saikrotiki akashindwa kukamatwa au kusababisha upelelezi dhidi ya mshtakiwa usifanyike vizuri atachukuliwa hatua za kinidhamu mbali na kuwajibika kwa kosa la jinai kama litakavyojitokeza kuhusiana na kutotimiza wajibu wake au kutokana na kuzembea huko.

(4) Endapo kutatokea ukinzani baina ya masharti ya kifungu hiki ya yake ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sheria hii itapewa kipaumbele.

SEHEMU YA TANO
UFILISI WA MALI ZILIZOTOKANA NA BIASHARA YA DAWA
ZA KULEVYA

Ufilisi wa mali
Sura 256

49.-(1) Kwa kuzingatia Sehemu hii, pale mtu anapotiwa hatiani kwa kosa lililopo Sehemu ya Tatu, mali anazomiliki kuanzia tarehe aliyotiwa hatiani kwa kosa linalofanana au alizopata baada ya tarehe hiyo, zitafilisiwa na Serikali kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utaifishaji wa Mali Zinazohusiana na Uhalifu.

(2) Masharti ya kifungu kidogo cha (1) yatatumika-

(a) mtu yoyote aliyetiwa hatiani kwa kosa chini ya Sheria hii;

(b) mtu yeyote aliyetiwa hatiani kwa kosa linalofanana nje ya Jamhuri ya Muungano na mahakama yenye uwezo wa kisheria katika mashauri ya jinai.

(c) kila mshirika wa mtu anayetajwa kwenye aya za (a) na (b).

(3) Kwa madhumuni ya Sehemu hii, kama muktadha unahitaji vinginevyo-

“mshirika” maana yake ni-

(a) mtu yeyote ambaye alikuwa au ni msimamizi wa shughuli au mtunza fedha wa mtu aliyetiwa hatiani chini ya kifungu hiki;

(b) madhumuni wa dhamana yoyote, ambapo-

(i) dhamana imewekwa na mtu huyo;
au

- (ii) thamani ya raslimali zilizochangiwa na mtu huyo zikiwemo thamani ya mali, kama zipo, zilichangiwa na yeye awali kwenye dhamana kwa kiasi si chini ya asiliamia ishirini ya thamani ya mali za dhamana.

(4) Mali haitafilisiwa chini ya Sheria hii iwapo mali hiyo ilipatikana na mtu ambaye masharti ya Sheria hii yalitumika, miaka mitano kabla ya tarehe ya kushtakiwa kwa kosa linalohusiana na biashara haramu ya dawa za kulevya.

(5) Iwapo afisa aliyeidhinishwa kwa maandishi anafikiri kuwa mali yoyote ya mtu huyo inashikiliwa kwa niaba yake na mtu mwingine, afisa huyo ataagiza mtu huyo apeleke mali hizo kwa lengo la kutaifishwa.

Katazo la kushikilia mali iliyopatikana kwa njia zisizo halali

50.-(1) Mtu haruhusiwi kushikilia mali iliyopatikana isivyo halali, aidha yeye binafsi au kwa kumtumia mtu mwingine.

(2) Endapo mtu anashikilia mali zilizopatikana isivyo halali kinyume na kifungu kidogo(1), mali hizo zitafilisiwa kwa mujibu wa Sheria ya Utaifishaji Mali zinazohusiana na Uhalifu.

Mamlaka ya kuagiza kufanyika kwa uchunguzi au ukaguzi

51.-(1)Mamlaka inaweza kumuagiza afisa yeyote kumhoji, kumpeleleza au kufanyia uchunguzi mtu au kikundi cha watu kama itakavyoona inafaa.

(2) Afisa aliyeidhinishwa na Mamlaka, anaweza baada ya kupata taarifa za mtu yeyote anayehusiana na Sehemu hii, anashtakiwa kwa kufanya kosa lolote iwe ni katika Jamhuri ya Muungano au nje ya nchi ataendelea na hatua zote muhimu za kufuatilia

na kutambua kila aina ya mali alizopata kutokana na uhalifu.

(3) Endapo Afisa anapokuwa anahoji au kupeleleza, kuchunguza, au chini ya kifungu kidogo cha (1), ana sababu za kuamini pasipo shaka kuwa mali yoyote inayohusiana na uchunguzi au upelelezi au ukaguzi uliofanyika kwa njia ya uhalifu na kuna uwezekano mali hizo zikafichwa, kuhamishwa au kutumika kwa njia yoyote na kuweza kukwamisha kazi ya kutaifisha mali hizo chini ya sehemu hii anaweza kutoa amri ya kukamatwa kwa mali hizo.

(4) Endapo mali husika kulingana na kifungu kidogo cha (3) zitahamishwa, uhamishaji huo utakuwa batili.

